



وَسَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَاءَلُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيُسْتَأْتِفُنَهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَخْلُقُونَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُخَيِّنَنَّهُمْ هُمْ دِيَرُ الْيَوْمِ أَرْضَنِي لَهُمْ وَلَيُبَدِّلُنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Toleo: 1445/11 H

Alhamisi, 4 Ramadhan 1445 H

14/03/2024 M

Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi Kenya

[إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Baqara 2: 156]
(Imetafsiriwa)

Kwa imani thabiti na kujisalimisha kikamilifu kwa kudra ya Mwenyezi Mungu (swt), **Hizb ut Tahrir / Kenya** inaomboleza kwa Umma wa Kiislamu kwa jumla na watu wa Kenya hasa;

Ustadh Said Salim Ali

(Mwenyezi Mungu amrehemu) aliyefariki mnamo siku ya Alhamisi, tarehe 14 Machi 2024, baada ya kushambuliwa na majambazi.

Akiwa kama Ustadh na Imam, Ustadh Said alijiunga na Hizb ut Tahrir - chama cha Kiislamu cha kimfumo cha kilimwengu ambacho kinabeba ulinganizi adhimu wa kuregesha maisha kamili ya Kiislamu kuititia kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Mtume (saw). Ingawa, na sisi hatumtakasi yejote mbele ya Mwenyezi Mungu (swt), tunashuhudia kwamba alikuwa akitekeleza kujitolea kwake kwa Da'awa.

Hakika nyoyo zetu zinahuzunika, macho yetu yanabubujika machozi kwa msiba huu mkubwa wa baba na ndugu yetu, Ewe Mwenyezi Mungu, mrehemu na umsamehe. Ewe Mwenyezi Mungu, yakirimu mapokezi yake, na upanue muingio wake.

Mwisho, tunapenda kutuma rambirambi zetu za dhati kwa familia yake tukimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu (swt) awalipe malipo makubwa, na awape subira, ujasiri na faraja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu abadilishe makaazi yake kwa makaazi bora, na familia yake kwa familia bora, na atukusanye sisi na yeje chini ya bendera ya Mtume (saw) Siku ya Kiyama.

Shabani Mwalimu
Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir
Kenya